

Februari 4, 2009

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Bado Siku 10 Tu Mwisho wa Kutuma Maombi ya Ruzuku kwa Waandishi wa Habari

Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (Tanzania Media Fund – TMF) unawakumbusha waandishi wa habari hususan wanaoomba ruzuku za mikoani (Regional Grants) na za upeo mpana (Strategic Capacity Grants) kuwa bado siku 10 tu kufikia tarehe ya mwisho wa kutuma maombi ambayo ni 15/2/2009. Ikumbukwe kwamba baada ya tarehe hiyo tutaendelea kupokea maombi ya ruzuku za chap chap na za taasisi tu.

Tayari TMF imepokea maombi 72 ya waandishi mmoja mmoja. Mikoa mitatu iliyoongoza kutuma maombi ni Ruvuma (19), Dar es Salaam (19) na Mwanza (8). Miongoni mwa walioomba 46 ni wanaume na 26 ni wanawake, hivyo tunawahamasisha waandishi wa habari wanawake kuomba ruzuku. Kwa kuwa TMF inatoa ruzuku kiushindani ili kukuza ubora wa habari, tunahitaji maombi mengi zaidi na yenye viwango vya ubora. Maombi yanayosisimua, yenye ubunifu wa wazo la habari litakaloanzisha mjadala wa kujenga jamii yetu.

TMF imeandaa mjadala wa wazi wenye nia ya kuwawezesha waandishi wa habari na wahariri namna ya kukidhi ubora unaohitajika wa maombi ya ruzuku. Mjadala huu utafanyikia ofisi za TMF Dar es Salaam, Ijumaa, Februari 6, 2009, kuanzia saa 4 asubuhi mpaka saa 6 mchana. Unataka kujua zaidi namna ya kuomba ruzuku kwa viwango vya ubora unaotakiwa, kuuliza maswali ya msingi na kujengwa namna ya kubuni wazo la habari litakalosisimua? Karibu uungane na wenzako.

Maofisa wa TMF watakuwepo kukushirikisha aina ya maombi yanayokidhi viwango na kujibu maswali yako. Iwapo unavutiwa kuja tafadhali piga simu namba 2601082 kujisajili.

Tembelea tovuti yetu www.tmf.or.tz ili ujue TMF ni nini, nani anaweza kuomba ruzuku, Namna ya kutuma maombi na mengineyo.

Ofisi za TMF zipo Masaki, barabara ya Chole, zilizopo pia ofisi za SNV

Imetayarishwa na:

Ernest Sungura

Meneja wa Programu

Tumekusudia tupate maombi yenye uhalisia wa wazo la habari. Wazo linalosimama likiwa limeshinda mawazo mengine ya habari kwa uhalisia wake. Wazo la habari ambalo ni mahsusi likitanguliwa na utafiti wa awali unaohitabika katika maombi ya ruzuku.

Tanzania Media Fund